


KIJJI KITAPATA NINI KUTOKANA NA UVUNAJI WA MISITU ILIYO NDANI YA MIPAKA YA KIJJI?

Faida za kutenga maeneo kuwa misitu wa kijiji



Uvunaji kwenye eneo lililotengwa:

Kijiji kina haki ya kupata asilimia mia moja (100%) ya mapato yote yanayotokana na uvunaji endelevu unaofanyika katika eneo hili la la msitu. Kibali hutolewa na Halmashauri ya Kijiji husika na uvunaji husimamiwa na kamati ya maliasili ya kijiji husika kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.

Uvunaji kwenye eneo lisilotengwa:

Mapato yote yanayotokana na uvunaji unaofanyika kwenye msitu huu ni mali ya Serikali kuu au Halmashauri ya Wilaya kwa asilimia mia moja (100%) na kibali cha uvunaji hutolewa na kamati ya uvunaji ya wilaya kupitia kwa Halmashauri ya kijiji husika.

Ni vizuri kijiji kikatenga na kusimamia eneo lote la misitu iliyo ndani ya mipaka ya kijiji ili iweze kupata asilimia mia moja ya mapato yanayotokana na misitu hiyo kwa ajili ya shughuli za mandeleo ya kijiji na uhifadhi wa misitu

Imeandaliwa na Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA) kwa Ufadhili wa Mradi wa Kuongeza Mnyororo wa Thamani ya Mazao ya Misitu Tanzania Kwa Mawasiliano zaidi: Mkurugenzi Mtendaji; Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA); S.L.P 21522 Dar-es-Salaam – Tanzania; tovuti: www.mjumita.org barua pepe: mjumitaorg@mjumita.org

Kwa ufadhili wa ushirikiano wa Tanzania na Finland

